OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA-TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI KEMAMBO,
S.L.P 401 TARIME,
TAREHE ……..

Kumb. Na.kss/join/ 2021/____
Jina la mwanafunzi. ……
S.L.P ……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KEMAMBO WILAYA YA TARIME MKOA WA MARA MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI

Uongozi wa shule ya sekondari Kemambo unayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari KEMAMBO ipo umbali wa kilometa26 kusini mashariki mwa Halmashauri ya wilaya ya Tarime. Usafiri wa GARI kutoka mjini TARIME Unapatikana katika kituo cha mabasi cha TARIME Nauli ni Tsh.5000/= Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021 Ndani ya siku kumi na nne.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 sare za shule

a) Sare ya shule hii ni suruali mbili (nyeusi), soksi nyeusi na shati nyeupe kwa wavulana. ***suruali nadhifu chini upana inch 18.***
b) Sketi mbili nyeusi, soksi nyeupe kwa wasichana na shati nyeupe, Maelezo ya mishono ***marinda sita kwa wasichana.***
c) Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule.
d) Sare ya michezo kwa shule hii ni ***truck suti ya bluu*** kwa wavulana na wasichana na Raba .
e) Sweta ya rangi ya bluu
f) Viatu rangi nyeusi vyenye kamba

Nb.kitambaa cha suruali na sketi kiwe nyeusi iliyokoza namba moja.

2.2 i. Daftari, kaunta book quire 2 tisa (9) kalamu na mkebe wa hesabu
ii. File kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake za kitaaluma shuleni
iii. picha ya passport size moja.

Nkutakia maandalizi mema ya kujiunga nasi.

Wako

_____
MATINDE R. GIMONGE
MKUU WA SHULE

Mawasiliano -0686046770

2.3 Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzungatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preaparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na;
i) Kutunza mali za umma.

2.4 **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa na kusimamishwa shule**

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi.

2.4 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

a) 'Medical examination Form' ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MZAZI WAKE PAMOJA NA AHADI YA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO.

1. Jina kamili la mwanafunzi ……..
2. Tarehe ya kuzaliwa ……
3. Shule aliyotoka ……
4. Mwanafunzi anatoka mtaa wa/ kijiji cha/ mji wa ……..
5. Kata ya ……
6. Jina kamili la Baba/ Mlezi ……..
7. Jina kamili la mama ……
8. Anuani kamili ya Baba/Mlezi ……..
9. Kazi afanyayo Baba/Mlezi ……..
10. Nina wazazi wote/ Mzazi mmoja/ Sina wazazi wote (yupo Baba/Mama)
11. **Ahadi.** Mimi (jina la mwanafunzi) ……..
    Nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii. Naahidi kutii sheria na taratibu zote kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule. Sitashiriki katika migomo, fujo na makosa yote ya jinai.

    Tarehe …….. Sahihi ya mwanafunzi ……
12. Mimi (jjina la mzazi/Mlezi) ……..
    Ambaye ni mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi ……
    Nimeyasoma na kuelewa masharti na sheria zote za shule hii ambako mwanangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kushirikiana na uongozi wa shule hii katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia bora wa Taifa letu.

    Tarehe …….. Sahihi ya Mzazi/Mlezi ……..

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT-PORALG

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

FULL NAME ……..
AGE …….. HEIGHT …….. WEIGHT ……
1. BLOOD COUNT ……
2. STOOOL EXAMINATION ……..
3. URINALYSIS ……..
4. SYMPHILIANSIS AND OTHER ……
5. T.B AND LEPROSEYTEST……..
6. EYE TEST ……..
7. EARS ……..
8. CHEST ……
9. ABDOMEN TEST (GIRLS) ……
10. ABDOMEN ……..
11. PLANO TEST (GIRLS) ……..
12. SPLEEN ……..

I. CERTIFY THAT THE ABOVE NAMED STUDENT IS FIT/UNFIT TO PARSUE SECONDARY EDUCATION

Signature ……..
Designature ……
Station ……
Date ……..